# LEARNING BY EAR 2012

## “Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”

## EPISODE 1: “Haikuwa mimi”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: KAPAKA AKIFANYA KAZI KATIKA DUKA LA KUUZA JUMLA**

- **Kapaka (mume, 25)**
- **Bwana Patel (mume, 40, lafudhi ya kihindi)**
- **Umati (watu 3 - 4 , jinsia na umri mchanganyiko)**
- **Wanunuzi (umri na jinsia sio muhimu)**
- **Msimulizi**

**SCENE TWO: VALERIE NA IRENE KATIKA KIHOTELI CHA CHUONI**

- **Valerie (Mke, 19)**
- **Irene (mke, 19)**
- **Msimulizi**

## SCENE THREE: MALEMBA NA CHUMBA KIJIJINI

- **Malemba (mke, 35)**
- **Chumba (mume, 16)**

**Msimulizi**

## SCENE FOUR: KAPAKA OFISINI KWA PATEL

- **Kapaka (mume, 25)**
- **Mr. Patel (mume, 40)**

**UTANGULIZI:**

Hujambo msikilizaji, na karibu katika makala yetu mapya ya **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Jiunge nami katika vipindi kumi vijavyo, tutakapokueleza hadithi ambayo wengi wameiepuka, kuhusu watu wasiotambulika, kwa sababu kauli zao tumezitupilia mbali. Na wanapozungumza, hakuna anayewapa sikio, kwa sababu wamepewa kila aina ya majina, wenda wazimu, punguani, vichaa, makreki, mafyuzi na mengineyo mengi.

Hii ni riwaya inayoangazia matatizo wayapatayo wanaougua maradhi ya akili barani Afrika. Tutakutana na Kapaka, kijana mwenye ari na mtazamo mzuri kuhusiana na familia yake – mpaka kulipoalika mbarika. Kisha kuna Valerie, mwanafunzi wa taaluma ya uuguzi ambaye ghafla anachanganyikiwa akili. Halafu kuna Chumba, kijana wa miaka 16 ambaye hajawahi kuuona mlango wa shule kwa ajili ya kuugua maradhi ya akili. Familia zao na jamii zao zinawachukuliaje? Je, mfumo wa matibabu na afya umejiandaa vipi kuwahudumia? Haya yote na mengineyo utayapata katika hadithi, **“Bado ningali mwanadamu”.**

Kipindi chetu cha kwanza kinaitwa, “**Haikuwa mimi”** Tunaanza katika duka kubwa la mahitaji liitwalo kwa kiingereza “All in one supermarket”. Kapaka, ambae ameoa hivi karibuni na yupo na mke wake mjamzito, ni keshia katika duka hilo.

**SCENE ONE: KAPAKA WORKING AT THE SUPERMARKET**

1. **SFX:** **BUSY SUPERMARKET AMBIENCE**

2. **KAPAKA:** **(cheerful)** Habari ya mchana.

3. **MNUNUZI:** Salama nashukuru.

4. **SFX:** **BEEP SOUND AS GROCERIES ARE COUNTED ELECTRONICALLY**

5. **KAPAKA:** Jumla itakuwa 850

6. **SFX:** **MONEY HANDED OVER**

7. **KAPAKA:** Subiri bakshishi yako, tafadhali.

8. **SFX:** **MONEY UNIT OPENED THEN COINS COUNTED**

9. **KAPAKA:** **(Still cheerful)** Karibu. Shukran kwa kununua bidhaa hapa “All in one”, tafadhali urudi tena wakati mwengine.

10. **MNUNUZI:** Bila shaka, kwaheri.

11. **KAPAKA:** **(to next customer)** Hujambo mama…

12. **SFX:** **TELEPHONE RINGS**

13. **KAPAKA:** Samahani, itanibidi nipokee hii simu. **(answers phone)** Kapaka hapa.

14. **PATEL:** **(Indian accent, on the phone)** Kapaka, haraka njoo “in my office”!

15. **KAPAKA:** Bwana Patel, kuna msururu mrefu wa wateja wanaohitaji kuhudumiwa.

16. **PATEL:** **(shouts)** Mimi pana jali bana, hata kama ni rais anangoja. Kuja afisini! Mara moja nasema!

17. **KAPAKA:** **(to clients)** Samahani, nimefunga kwa sasa. Nenda kwa keshia mwengine.

18. **SFX:** **COMPLAINTS AND CURSING FROM CROWD**

19. **SFX:** **PEOPLE MOVING TO OTHER CASHIER**

20. **MSIMULIZI:** Ilikuwa bayana kwa Kapaka na keshia wenzake kwamba bwana Patel alichukulia mteja kama mfalme. Kughadhabika kwa Patel kulimaanisha kuna jambo limeharibika mno. Kapaka alinyanyuka na kuelekea katika ofisi ya bosi wake, Patel. Kwengineko katika shule moja ya uuguzi ndani ya jiji, Valerie, mwanafunzi wa

uuguzi anapata chakula cha mchana na rafikiye Irene katika kihoteli kimoja hapo chuoni kwao…

**SCENE TWO: VALERIE NA IRENE KATIKA KIHOTELI HAPO CHUONI**

**21. ATMO:** **COLLEGE CANTEEN AMBIENCE**

**22. IRENE:** **(takes deep breath)** Fyu, nashukuru nimetoka chumba cha upasuaji. Sidhani kama ningependelea kufanya ajira hii. Valerie, ulitaka kuwa muuguzi wewe tangu utotoni?

**23. VALERIE:** (**absent-minded)** Nini! Upasuaji? Irene, nafikiri umefanya vyema. Unahitaji muda kuzoea. (**in pain)** Aaah!

**24. IRENE:** Uko sawa, Valerie? **(concerned)** Hata hukunisikia nimekuuliza nini, umenisikia kweli? Nimekuuliza kama ulitaka kuwa muuguzi.

**25. VALERIE:** **(strangely)** Mimi? Nesi? Hapana, labda daktari!

**26. IRENE:** **(confused)** Sawa, kwahivyo mbali na kuwa mwanafunzi bora wa unesi, sasa una azma ya kuwa daktari?

**27. VALERIE:** **(emphasis)** Mpasuaji wa ubongo! La ! Daktari! Mmmh… ndiyo! Nitapeana huduma juu angani.

**28. IRENE:** Unanishangaza, Valerie. Kula kitu basi, si ajabu kuchanganyikiwa kwako kwaletwa na njaa. Labda kutaondoka ukishiba.

**29. SFX:** **CUTLERY SOUNDS AS WHEN PEOPLE EAT A MEAL**

**30. SFX:** **CUTERLY PLACED DOWN, PLATE PUSHED AWAY**

**31. VALERIE:** Siwezi tena kula. Nimepoteza hamu ya chakula**.**

**32. IRENE:** Valerie, una uhakika uko sawa?

**33. VALERIE:** **(brushes it off)** Irene, tangu lini ukawa daktari? Mimi ndimi daktari!
**(short pause then calmly)** Hapana, usihofu rafiki yangu. Niko sawa.

**34. IRENE:** Val, una hakika? Kwa dakika chache pale, nafikiri ulikuwa huko na mimi. Sikuwa naelewa usemacho. Tafadhali pata dawa na ujipumzishe, tuko kipindi muhimu sana katika

masomo yetu hapa chuoni. Huwezi kukosa masomo.

**35. VALERIE:** Sawa, sawa Irene…nitameza dawa. **(jokes)** Umenisamehe, Mama?

**36. IRENE:** Sikutanii, Valerie!

**37. VALERIE:** **(suddenly angry)** Sawa, hata mimi sina mzaha! Endelea na chakula chako.

**38. SFX:** **CHAIR BEING PULLED BACK**

**39. IRENE:** **(shocked)** Valerie - subiri! Sikunuia kukuudhi. Valerie…!!!

**40. SFX:** **ANOTHER CHAIR BEING PULLED BACK**

**41. MSIMULIZI:** Kama moto kichakani, huanza na cheche moja. Wakati mwengine moto huo huchukuwa miezi au siku nyingi kudhibitiwa. Tena iwapo una vifaa muhimu vya kuukabili. Valerie bila shaka hayuko sawa. Atachukua hatua gani kabla hajalipuka? Tutajionea. Lakini tutoke katika maisha ya jijini na tuelekee kijijini. Katika kijumba kimoja kikuukuu kilichoadimika watu. Malemba, mlezi wa pekee, anafagia uwanja wa kijumba hicho. Karibu na hapo kipo kijumba kidogo cha udongo, na ndani anajisitiri kijana wa Malemba's mwenye umri wa miaka 16 aitwae Chumba. Amefungwa kwenye kitanda cha teremka tukaze huku akilalia mkeka tu. Akili za Chumba zina matatizo, upungufu huu umempa kutotangamana na watu. Lakini

mamake Malemba hajui lolote kuhusu maradhi haya, kwa hivyo ana maoni tofauti kuhusu hali hii ya mwanae. Usiondoe sikio lako, mpenzi msikilizaji.

**SCENE THREE: MALEMBA AND CHUMBA IN THE VILLAGE**

42. **ATMO:** **VILLAGE AMBIENCE, OUTSIDE**

43. **MALEMBA:** **(Singing a sad song)**

44. **SFX:** **TRADITIONAL BROOM SWEEPING GROUND**

45. **CHUMBA:** **(screaming words that can't be understood)**

46. **SFX:** **FEET RUSHING AS MALEMBA RUSHES INTO THE HUT**

47. **MALEMBA:** **(rushes in)** Muacheni mwanangu, nyie pepo wachafu! Nendeni! Rudini mlikotoka! Muacheni!

48. **CHUMBA:** **(makes more noises)**

49. **MALEMBA:** Basi baba.., Chumba, wameenda. Washaondoka sasa. Tulia kijana wangu, tulia. Mamako niko hapa…sssssh.
**(calms him down with a song)**

**Silence**

**50. CHUMBA: (starts to scream again)**

**51. MALEMBA:** Mamako nimefika, Mama niko hapa, Mama haondoki ….
**(starts to weep)** Chumba, hebu nyamaza. Acha kupiga mayowe, mwanangu. Mama mimi niko hapa?

**52. MSIMULIZI:** Vilio kama vya Malemba kwenye vijumba duni, ni vingi mno barani Afrika. Hivi kweli watu kama hawa kina Chumba wana msaada wowote? Watasaidiwa vipi kama wanabaguliwa, hawashughulikiwi na wanatengwa? Endelea nasi tupeleleze pamoja. Tunaporudi katika lile duka la jumla, Kapaka amesimama mkabala na muajiri wake, bwana Patel.

**<u>SCENE FOUR: KAPAKA NDANI YA OFISI YA PATEL</u>**

**53. SFX: DOOR BEING CLOSED**

**54. PATEL:** **(firmly)** Kapaka, Wewe huna kazi! Kwisha!

**55. KAPAKA:** **(utterly shocked)** Kwanini!? Nimefutwa kazi? Bwana Patel, huu si mzaha?

**56. PATEL:** **(seriously)** Sikiliza maneno yangu bizuri **(pronounces word after word)** ni.. me.. futa wewe kazi! Tena iko mara moja, wewe hapana

iko mafanyakazi tena hapa dukani ya jumla ya “All in wan”. Elewa mimi? Toa nguo yako ya kazi na kipande!

**57. KAPAKA:** **(confused)** Sielewi. Kwanini ninafukuzwa kazi? Nimekosea nini.

**58. PATEL:** Oh wewe! Najua kuigiza sana, kwenda cheza Bollywood… wewe naiba mapesa yangu ya jana halafu naweza kusimama mbele ya mimi na kusema Habana yuwa! Bahati yako mimi hapana eleza polisi...

**59. KAPAKA:** Mimi? Niliiba pesa? Patel, nakuapia…

**60. PATEL:** *Bwana*. Patel! Tena panaita mimi Patel kama chauro! mimi apana iko rafiki yako. Mimi iko bosi yako. Unafanya paka nakosea... mimi ilikuwa bosi yako pana sasa....

**61. KAPAKA:** Bwana Patel, unanijuwa vyema. Nimekufanyia kazi takriban miaka mitatu sasa, sijalalama wala kulalamikiwa. Isitoshe, nimeoa juzi, mkewangu atapata mtoto muda wowote kutoka sasa. Kwanini nifanye kitu kitakachosababisha niharibu kazi yangu? Haya ni makosa! Sikuwahi! Siye mimi! Kuna makosa!

62. **PATEL:** Makosa kubwa ni mimi kuamini wewe na kuandika wewe kazi. Sasa pana haribu makati yangu. Peana kitu zote napewa hapa ndani ya dukani yangu.

63. **KAPAKA:** Haikuwa mimi, ninaapa. Sijawahi hata kukuiba senti moja. Haikuwa mimi!

64. **PATEL:** Kweli tupu, hapana wewe. Pesa namea maguu na makono halafu najitoa menyewe kwenye kiengi na kutoweka. Kapaka, afadhli wazazi yako naita wewe Kamwizi... toka bana!

65. **KAPAKA:** **(in denial)** Haikuwa mimi, siye mimi. La.. la .. sikuwahi kufanya hivyo! Haikuwa mimi.

66. **PATEL:** Asante kwa kazi yako. Babai!

67. **SFX:** **DOOR CLOSED ABRUPTLY**

**HITIMISHO:**

Basi hayo yanatamatisha kipindi chetu cha kwanza, katika hadithi hii ya matatizo yawapatayo wanaougua maradhi ya akili barani Afrika. Ni yapi yaliosalia kwa Kapaka baada ya kufutwa kazi? Hali hii ya Valerie kweli itazidi kusambaratika? Na kule kijijini, ni kweli Chumba kapagawa na mapepo? Na kama sivyo, anaugua nini? Je watu kama hawa, wanaweza kupona kweli? Haya na mengine mengi ni katika vipindi vijavyo.
Kama unataka kusikiliza tena kipindi hiki basi tembelea wavuti wetu dw.de/ lbe. Mpaka wakati mwengine tena. Kwaheri.